Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3591

East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 8, Issue 2, 2025
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EANSO
EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

Original Article

Mkakati Wa Uhalalishaji wa Kimamlaka katika Hotuba Teule za Marais wa Tanzania katika Vikao vya Pamoja vya Mabunge ya Kitaifa, Kenya

Sammy Dimbu[1*], *Prof. John Kobia, PhD*[1] *na Dkt. Mary Kanyua, PhD*[1]

[1] Chuo Kikuu cha Chuka, S.L.P 109, Chuka, Kenya.
[*] ORCID ID; https://orcid.org/000-0001-5070-6915; Barua pepe ya mawasiliano: dimbuliana@gmail.com

DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3591

Tarehe ya Uchapishaji:

05 Septemba 2025

Istilahi Muhimu:

Hotuba teule, Kimamlaka, Mkakati wa Uhalalishaji, Marais wa Tanzania na vikao vya pamoja vya Mabunge ya Kitaifa.

IKISIRI

Makala hii ilihusu uhalalishaji wa kimamlaka katika hotuba teule za Marais wa Tanzania katika vikao vya pamoja vya Mabunge ya Kitaifa nchini Kenya. Nadharia iliyoongoza makala hii ni Uchanganuzi Makinifu wa diskosi. Nadharia hii hudokeza kuwa lugha kivyake haina mamlaka, bali huyapata itumiwapo na wenye mamlaka katika miundo ya kijamii. Sampuli ya makala hii ilipakuliwa kutoka kumbukumbu za kudumu za Mabunge ya Kitaifa nchini Kenya zilizoko mtandaoni. Diskosi za hotuba teule za Marais Jakaya Kikwete na Samia Suluhu zilizo sampuli ya makala hii ni zile zilizowasilishwa kati ya miaka (2013-2022). Kipindi hiki ni awamu ya 11 na awamu ya pili na tatu ya Mabunge ya Kitaifa na Seneti nchini Kenya. Jumla ya hotuba mbili ziliteuliwa kimakusudi kwa kujikita kwenye mbinu ya uchanganuzi wa yaliyomo. Kifaa cha utafiti kilichotumika katika ukusanyaji wa data ni orodha ya ukaguzi. Muundo wa kimaelezo ulitumika katika kukusanya, kuchambua na kuwasilisha matokeo ya makala. Data ya makala hii ilikusanywa kutokana na mchakato wa usomaji wa kina wa hotuba teule. Matokeo ya makala hii yalidhihirisha kuwa mikakati ya kibinafsi, wataalamu, mfano wa kuigwa, yasiyo binafsi, upatanishi wa kimila. Makala hii ilipendekeza kuwa utafiti wa baadaye ufanywe kuhusu namna vipengele vya mkakati wa uhalalishaji wa mamlaka hutambulisha wahutubu katika hotuba za kisiasa.

APA CITATION

Dimbu, S., Kobia, J. & Kanyua, M. (2025). Mkakati Wa Uhalalishaji wa Kimamlaka katika Hotuba Teule za Marais wa Tanzania katika Vikao vya Pamoja vya Mabunge ya Kitaifa, Kenya. *East African Journal of Swahili Studies*, *8*(2), 265-282. https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3591

CHICAGO CITATION

Dimbu, Sammy, John Kobia and Mary Kanyua. 2025. "Mkakati Wa Uhalalishaji wa Kimamlaka katika Hotuba Teule za Marais wa Tanzania katika Vikao vya Pamoja vya Mabunge ya Kitaifa, Kenya". *East African Journal of Swahili Studies* 8 (2), 265-282. https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3591

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3591

HARVARD CITATION
Dimbu, S., Kobia, J. & Kanyua, M. (2025) "Mkakati Wa Uhalalishaji wa Kimamlaka katika Hotuba Teule za Marais wa Tanzania katika Vikao vya Pamoja vya Mabunge ya Kitaifa, Kenya", *East African Journal of Swahili Studies*, 8(2), pp. 265-282. doi: 10.37284/jammk.8.2.3591

IEEE CITATION
S., Dimbu, J., Kobia & M., Kanyua "Mkakati Wa Uhalalishaji wa Kimamlaka katika Hotuba Teule za Marais wa Tanzania katika Vikao vya Pamoja vya Mabunge ya Kitaifa, Kenya", *EAJSS*, vol. 8, no. 2, pp. 265-282, Sep. 2025.

MLA CITATION
Dimbu, Sammy, John Kobia & Mary Kanyua. "Mkakati Wa Uhalalishaji wa Kimamlaka katika Hotuba Teule za Marais wa Tanzania katika Vikao vya Pamoja vya Mabunge ya Kitaifa, Kenya". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 8, no. 2, Sep. 2025, pp. 265-282, doi:10.37284/jammk.8.2.3591.

UTANGULIZI

Makala hii ililenga kufafanua mkakati wa uhalalishaji wa kimamlaka katika hotuba za Marais Kikwete na Samia katika vikao vya pamoja vya Mabunge ya Kitaifa nchini Kenya. Makini ya kutafiti mkakati ya uhalalishaji ilitokana na namna lugha hutumiwa na wanasiasa, kudhibitisha matendo yao au kujenga utambulisho wa kijamii. Uhalalishaji ni dhana changamani yenye pande za kijamii-siasa, simiotiki na mazoea ya kijamii. Ina maana kuwa hutekeleza majukumu yake katika kiwango kama tukio la kijamii-kisiasa kama vile Marais Kikwete na Samia, mtindo wa hulka na mpangilio wa mandhari kama vile mandhari ya vikao vya pamoja vya Mabunge ya Kenya yaliyohutubiwa na Marais Kikwete na Samia. Aidha, usemi, diskosi na matumizi ya lugha kama ilivyo katika hotuba teule. Huwa kuna mwingilianao changamani baina ya pande hizi za uhalalishaji. Uhalalishaji katika diskosi za kisiasa hufafanua kinachosababisha raia wa jamii za mfumo wa kidemokrasia kutambua mamlaka, yaani mamlaka halali ya serikali na namna serikali hutafuta utiifu kutoka kwa watawaliwa (Kostova, 2020).

Hivyo uhalalishaji ni mfumo ambao kupitia kwake washiriki wa kijamii katika mchakato wa mawasiliano hutoa kibali cha kufanyika kwa kitendo au hulka katika jamii mahususi. Uhalalishaji ulitokea katika hotuba teule kupitia wahutubu wakifafanua maamuzi fulani, mawazo, au hulka walizohitaji ziungwe mkono na hadhira lengwa katika hotuba teule za Marais Kikwete na Samia. Mfumo huu wa uhalalishaji wa kimamlaka hutokana na mamlaka ya kisheria, kitamaduni, au mtu mwenye mamlaka ya kitaasisi (van Leeuwen, 2008). Uhalalishaji wa mamlaka ulikuwa mfumo ambao washiriki wa kijamii, taasisi au sera ulitumiwa na Marais Kikwete na Samia kutafuta ukubalifu na kutambuliwa. Hii ilitokana na uhalalishaji wa mamlaka ya kushinikiza utiifu wa hiari kuliko nguvu za kiimla. Yaani, uhalalishaji ni uthibitishaji wa hulka za mifumo yake ambayo huwekwa kupitia kwa hoja za kueleza tukio la kijamii.

Katika uchanganuzi makinifu wa diskosi, uhalalishaji wa mamlaka ni dhana kuu kwa sababu uchanganuzi huu hulenga kufichua jinsi mahusiano ya nguvu yanavyotekelezwa, kuzalishwa upya, na kudumishwa kupitia lugha na mazungumzo. Mamlaka, katika muktadha huu, si tu kuhusu nafasi rasmi, bali pia kuhusu ukubalifu, uhalali, na kukubaliwa kwa madai fulani, vitendo, au mipangilio ya kijamii (Fairclough, 1992). Kwa ujumla uhalalishaji ni mfumo ambao wahutubu hudhihirisha aina ya hulka ya kijamii na kitendo ambacho huhusishwa na lengo, ambalo huhitaji kuungwa mkono wa hadhira. Ni haki ya watu kumtii mtu (Reyes, 2011).

Makala hii ilijikita katika sampuli ya hotuba za Marais Kikwete na Samia katika vikao vya pamoja vya Mabunge ya Kitaifa nchini Kenya. Hotuba za kisiasa kama sampuli ya makala hii ni mandhari ya kimakusudi ya mtagusano baina ya hadhira na mhutubu, ambapo lengo la mawasiliano la mhutubu ni kushawishi hadhira kukubali na kuunga mkono

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3591

mwonoulimwengu wake, na mapendekezo yake. Kwa mujibu wa Bayley (2004) tafiti zinazohusu bunge zimepuuza kufanya tafiti kuhusu diskosi za bunge kiisimu licha ya bunge kuwa taasisi inayozungumza. Kulikuwa na haja ya kuchunguza hotuba teule kwa kutumia uchanganuzi makinifu wa diskosi.

MAPITIO YA MAANDISHI

Kwa mujibu wa Cap (2008), wahutubu wa kisiasa hutumia mikakati ya uhalalishaji ili kustawisha matendo yao. Ni kutokana na matukio katika hotuba hizi, viongozi wa kisiasa huunga mkono ajenda zao za kisiasa, kuendeleza au kubadili taifa nzima au hata kanda (Reyes, 2011). Mtaaluma Reyes (keshatajwa) alitafitia mikakati ya uhalalishaji katika diskosi za kisiasa, "kutoka kwa maneno hadi kwa matendo" katika hotuba za Marais wa Marekani. Mikakati ya uhalalishaji iliyobainishwa ni hisia, maono kuhusu siku za usoni, matokeo ya kitendo fulani na maoni ya wataalamu. Aidha, utafiti wake ulieleza kuwa Rais George W. Bush na Barack Obama kati ya miaka ya 2007 na 2009 mtawalia walitumia mikakati ya uhalalishaji mbalimbali. Mikakati hii ilitumika kupata uungwaji mkono wa kuendelea kuwepo kwa wanajeshi wa nchi ya Marekani nchini Iraq na Afghanistan.

Sawia na utafiti wa Reyes (keshatajwa), makala hii ilitafitia diskosi za kisiasa na utafiti wake ulikuwa dira katika uchanganuzi wa data iliyohusu uhalalishaji. Hii ni kwa sababu nadharia ya uchanganuzi makinifu wa diskosi ilitumiwa katika makala hii. Utafiti wa Reyes (keshatajwa) ulifaa makala hii katika kufafanua namna Marais Kikwete na Samia walitumia mikakati ya uhalalishaji ya mamlaka kuunga mkono masuala ambayo yalikosa mvuto kwa hadhira. Tofauti ni kuwa sampuli ya makala hii ni hotuba za Marais Kikwete na Samia katika vikao vya pamoja vya Mabunge ya Kitaifa nchini Kenya.

Hotuba ni sehemu ya diskosi iliyoandikwa na lengo lake si kuhamasisha tu bali ni mchakato wa kulinda na kupigania maslahi ya mwanasiasa husika (van Dijk, 1998). Utafiti wa Jamil (2014) uliangazia mikakati ya kuharamisha iliyotumiwa na Hosni Mubarak na Ben Ali, Marais wa nchi za Misri na Tunisia mtawalia mwaka wa 2011 ili kuibua hisia fulani. Mikakati hii ilitambuliwa kupitia mikakati ya uhalalishaji ambayo ni pamoja na mamlaka, matokeo, maadili na usimulizi. Utafiti wa Jamil (keshatajwa) ulidhihirisha kuwa katika mtazamo wa kijamii na kisiasa mzozo wa kimaslahi kati ya serikali na wananchi ni suala la kawaida. Utafiti wa Jamil (keshatajwa) haukuangazia lugha kama chombo cha mawasiliano tu, bali chombo cha kuwafaa wanasiasa katika shughuli zao za kisiasa. Hii ni kwa sababu ilihalalisha masuala ambayo yalionekana kulinda maslahi ya uongozi.

Utafiti wa Jamil (keshatajwa) ulifaa makala hii katika kuchanganua mikakati mbalimbali ya uhalalishaji iliyotumiwa katika hotuba teule. Mikakati ya mamlaka, ya kimaadili na hisia ilihalalisha maslahi ya "sisi" huku ikiharamisha ya "wao" ili kulinda maslahi ya kihejemonia ya kundi tawala. Aidha, kueleza namna Marais Kikwete na Samia walivyotumia mikakati hii kuirai hadhira kukumbatia sera za uongozi wao kuhusu uhusiano wa Mataifa ya Kenya na Tanzania. Hatimaye, kufafanua namna mahitimisho na mapendekezo ya Marais Kikwete na Samia katika hotuba teule yalivyokuwa muhimu kuzingatiwa na hadhira lengwa ili wasiunge mkono masuala yanayoweza kuvuruga uhusiano wa kikanda. Hata hivyo, utafiti wa Jamil (keshatajwa), ulibainisha mikakati ya uhalalishaji ya matokeo na usimulizi ambayo haikuangaziwa katika matokeo ya utafiti huu. Makala hii ilijikita katika mkakati ya uhalalishaji mamlaka.

MISINGI YA NADHARIA

Nadharia iliyoongoza makala hii ni Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi. Kwa mujibu wa Wodak na Meyer (2001) nadharia ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi iliasisiwa mwanzo wa mwongo wa 1990 na kundi la wasomi mbalimbali. Tafiti

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3591

zinazoegemezwa katika nadharia ya uchanganuzi makinifu wa diskosi huchukua mitazamo mbalimbali ya kisarufi. Dhana muhimu kama vile diskosi, makinifu, itikadi na mamlaka hutofautiana kulingana na mitazamo hii (van Dijk, 2002). Kwa mujibu wa van Dijk (1995) mitazamo ya uwingipande, wingiviwango, wingitaaluma na mwingilianotaaluma hupendekezwa katika uchanganuzi wa diskosi. Uhakiki wowote ule lazima ubainishe mtazamo uliozingatiwa. Ina maana kuwa uchanganuzi makinifu wa diskosi si mfumo funge. Mitazamo ya nadharia hii hufafanua diskosi kuwa mchakato, ung'amuzi, na kumbukumbu za kijamii na kihistoria.

Mitazamo hii ilitumiwa katika kukusanya data, kuchambua data na kuwasilisha matokeo ya makala hii kutokana na sampuli ya hotuba teule. Uhalalishaji wa mamlaka katika hotuba teule uliangaziwa kama mchakato, ung'amuzi na kumbukumbu za kijamii na kihistoria kwa mujibu wa muktadha wa hotuba teule. Mihimili iliyoongoza makala hii ni diskosi huangazia changamoto za kijamii, mahusiano ya uwezo hukuzwa na mazoea ya kijamii, diskosi husheheni jamii na utamaduni, diskosi hutekeleza jukumu la kiitikadi, diskosi ni kumbukumbu za kihistoria, kuna uhusiano wa kimwingiliano kati ya usemi na jamii, uchanganuzi wa diskosi ni kutafsiri na kufafanua na diskosi ni aina ya tendo la kijamii.

MBINU ZA UTAFITI

Muundo uliochukuliwa katika makala hii ni wa kimaelezo kwa sababu data ilichambuliwa kiufasiri. Mada iliyotafitiwa si ya kitakwimu na haikufanyiwa hesabu. Uchanganuzi makinifu wa diskosi ni uchanganuzi wa kimaelezo wa vipengele vya kiisimu katika diskosi husika (Huckin na wengine, 2012). Mbinu ya usampulishaji wa kimakusudi hutumika katika utafiti wenye muundo wa kimaelezo kama huu (Bryman, 2016). Uteuzi wa sampuli kimakusudi ulimpa mtafiti fursa ya kuteua sampuli yenye data iliyohitajika na iliyojitosheleza, na hivyo kuwezesha kujibu maswali ya utafiti (Mugenda na Mugenda, 1999). Hotuba iliyoteuliwa kimakusudi ilikuwa ile iliyotolewa na Rais Kikwete tarehe 6/10/2015 katika kikao kilichoandaliwa kulingana na ilani ya Gazeti la Serikali ya Kenya nambari 7371 na 7372 tarehe 1/10/2015. Isitoshe, hotuba ya Rais Samia tarehe 5/5/2021 iliteuliwa kimakusudi. Hotuba hii ilitolewa katika kikao kilichoandaliwa kwa mujibu wa ilani nambari 4199 na 4200 ya Gazeti la Serikali ya Kenya, tarehe 3/5/2021. Vikao vya pamoja vya mabunge ya kitaifa nchini Kenya kati ya miaka (2013-2022) viliteuliwa kimakusudi.

MATOKEO YA UTAFITI

Uhalalishaji wa mamlaka ya kibinafsi, wataalamu, mfano wa kuigwa, yasiyo binafsi, upatanifu na kimila ulibainika katika data ya makala hii.

Binafsi

Mamlaka ya binafsi hutokana na hadhi ya mtu kwenye taasisi kulingana na michakato ya kijamii. Wenye mamlaka haya hawahitajiki kuthibitisha maamuzi yao***, "kwa sababu ninasema hivyo" na huhalalishwa kutokana na hadhi ya jamii au nafsi katika taasisi (van Leeuwen, 2008). Tazama hapa chini madondoo ya (31a) na (b) yanadhihirisha mamlaka ya binafsi katika hotuba teule:***

(31a) Nilipofika, Rais Kibaki akaniambia mambo mawili; kwanza, nimwambie Kofi Annan asiondoke kwani wakati huo walikuwa wameshavunja mazungumzo. Na, aliyeniletea ujumbe huo ni Moses Wetangula (ukurasa wa 6).

(b) Kama alivyosema Mhe. Spika, aliyewahi kuhutubia hapa ni Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, kutoka Tanzania na mimi ni wa pili (ukurasa wa 3).

Uhalalishaji wa binafsi katika dondoo la (31a) ulitokana na matumizi ya mofu {ni-} katika vitenzi "nilipofika" katika hotuba teule ya Rais Kikwete. Mofu hii ilimtambulisha Rais Kikwete kuwa mpatanishi wa ghasia za baada ya Uchaguzi wa mwaka 2007 nchini Kenya. Deiksisi "mimi" ilimtoa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3591

Rais Kikwete kutoka katika hali ya wakati huo wa kuhutubia na kumwakilisha katika njia iliyo rasmi zaidi, yaani kuwa mpatanishi na Rais wa Tanzania. Hali hii ilitokana na mahusiano ya uwezo kati ya Rais Kikwete na hadhira. Alipata mamlaka na ukubalifu kutokana na kujitolea kwake kuwa mpatanishi.

Dondoo la (31a) lilihalalisha kitendo cha Rais Kikwete kupatanisha pande pinzani baada ya uchaguzi wa mwaka 2007. Yaani, alichangia uwepo wa amani iliyoshuhudiwa nchini Kenya. Kwa mujibu wa van Dijk (2003) uchanganuzi makinifu wa diskosi huangazia nguvu, mamlaka, hejemonia, utabaka, uana, ubaguzi wa rangi, itikadi maslahi na muundo wa jamii. Hushughulikia namna matukio ya kijamii, mahusiano ya uwezo, turathi, itikadi, na ujitambulishaji unavyonasibishwa kwa watu na jamii kupitia miundo ya kiisimu. Uhalalishaji huu ulitokana na ujitoleaji nafsi ambao ulikuza ukubalifu na kumsawiri Rais Kikwete kama mkweli na mwenye msimamo thabiti. Hivyo, aliishawishi hadhira kukubali mtazamo wake kuhusu ghasia za baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2007 na kudhihirisha kuaminika kwake.

Uchanganuzi makinifu wa diskosi hujihusisha na uhalalishaji wa mahusiano ya mamlaka na utawala, ukubalifu na uzalishaji upya wa diskosi. Mofu {ni} ilitambulisha majukumu rasmi ya Rais Kikwete katika kutafuta mwafaka baada ya ghasia baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2007. Ujitambulishaji huu ulileta ushirikiano wa pamoja kati ya hadhira na yeye. Ikizingatiwa kuwa hadhira ilikuwa ya Wakenya waliofahamu ghasia hizi. Huu ulikuwa mkakati wa kushawishi hadhira kukubaliana naye na kuleta uaminifu upande wake. Aidha, ulikusudia kughilibu kwa kuficha au kupunguza hisia za kutokukabiliana kuhusu mchango wa Rais Kikwete katika mchakato wa mamlaka ya binafsi ilidhihirishwa na deiksisi ya nafsi *mimi*, ambayo iliwakilisha uhusiano wa kimamlaka kati ya nchi za Kenya na Tanzania.

Fairclough (1992) anadokeza kuwa diskosi ni shughuli za kijamii na hufafanuliwa katika muktadha wa itikadi na mamlaka. Vipengele vya kiitikadi vilivyofiche katika lugha sio rahisi kutambuliwe na njia pekee ya kuvitambua ni uchanganuzi makinifu wa diskosi. Rais Kikwete kwa njia isiyo ya moja kwa moja alihalalisha uhusiano wa kidiplomasia kati ya Kenya na Tanzania na mchango wake katika kutafuta maridhiano baada ya Uchaguzi wa mwaka 2007.

Aidha, katika dondoo la (31b) mamlaka ya binafsi ilidhihirishwa na deiksisi ya nafsi ya kwanza umoja mimi. Deiksisi hii ilimtambulisha Rais Samia kuwa mhutubu ambaye ni mgeni spesheli wa nchi ya Kenya. Hali hii ilitokana na ukweli yeye ni Rais wa pili kuwahi kuhutubia vikao vya pamoja vya Mabunge ya Kitaifa nchini Kenya. Kifungu, "...kutoka Tanzania na mimi ni wa pili..." kilisheheni jagoni za kuhalalisha. Jagoni za kuhalalisha zilikuwa kifaa cha mtagusano wa kijamii na kuendeleza mawasiliano ya wanakundi na mwingiliano wa kijamii. Marais wa nchi ya Tanzania hupewa nafasi maalumu kuhutubia vikao vya Mabunge ya Kitaifa nchini Kenya. Hata hivyo, Rais Samia alichokosa kuangazia ni kuwa kabla ya kuidhinishwa kwa Katiba ya mwaka 2010 na uchaguzi wa mwaka 2013, hapakuwepo na Mabunge mawili ya Kitaifa. Aidha, kanuni za bunge hazikuruhusu wageni maalumu kuhutubia bunge. Rais Samia alighilibu hadhira kwa kuficha au kupunguza hisia za kutokubaliana kwa kutotoa maelezo zaidi kwa nini alikuwa Rais wa pili kuhutubia Mabunge ya Kitaifa.

Uchanganuzi wa diskosi huchunguza usemi katika kuhalalisha, uzalishaji, na kupinga matumizi, utawala, na utofauti. Utafiti wa aina hii huchunguza vipengele vya kiisimu kutoka kwa semi za kisiasa, vilevile kugundua vipengele vilivyo nyuma ya usemi, kama vile mahusiano ya uwezo na itikadi (van Dijk, 2005). Hadhi ya Rais Samia kuwa rais wa nchi ya Tanzania ilimpa mamlaka sawa na mtangulizi wake Rais Kikwete. Hivyo, kuhutubia vikao vya pamoja vya Mabunge ya Kitaifa ilikuwa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3591

halali na hakuna aliyepaswa kupinga. Kwa mujibu wa van Dijk (1991) maarifa ya awali ni vipengele vya shughuli vya kisiasa na jamii. Maarifa katika dondoo hili yaliendeleza itikadi ya Rais Samia kuhusu kuwepo kwa uhusiano mzuri kati ya Mataifa ya Kenya na Tanzania.

Muktadha huathiri kile kinasemwa na watu na namna wanavyokisema (van Dijk, 2006). Maana ya mamlaka ya binafsi katika dondoo la (31b) ni kuwa Rais Samia alikuwa tayari kubadili sera ya uongozi nchini Tanzania kuwa kama ile ya Rais Kikwete. Kwa mujibu wa van Dijk (2001) uchanganuzi makinifu wa diskosi hujikita kwenye kilichoachwa kusemwa, kilichowachwa nje kupitia maana ambayo huhimiza utata. Hayati Rais Magufuli alikuwa madarakani katika awamu ya tano na uhusiano kati ya mataifa haya uliyumba. Kupitia dondoo la (31b) Rais Samia alikiri kuwa Hayati Magufuli hakuzuru Kenya. Aidha, uhusiano wa Kenya na Tanzania ungeimarika kama ulivyokuwa chini ya uongozi wa Rais Kikwete.

van Dijk (2001) anadokeza kuwa jamii huchanganuliwa katika kiwango cha muktadha na mtagusano katika vikundi, mpangilio wa kijamii na kiwango cha taasisi. Diskosi huhusiana na jamii kupitia uwasilishaji wa kijamii na washiriki wa muundo. Aidha, kupitia kudhihirika kwa uwakilishi wa miundo ya kijamii na washiriki wa jamii. Uchanganuzi wa diskosi sio uchanganuzi wa lugha tu, na ni nyanja zote ambazo itikadi hupenyeza. Miundo ya kijamii iliwapa Marais Kikwete na Samia hadhi ya urais katika madondoo ya (31a) na (b) ambayo iliwaweka katika mahusiano ya uwezo yaliyo juu kuliko hadhira.

Hadhi hii iliwapa fursa ya kutumia deiksisi za nafsi ya umoja katika kuhalalisha utambulishaji wao kama “Rais wa Tanzania, mpatanishi nchini Kenya” na “Rais wa Tanzania ambaye alikuwa mhutubu katika Mabunge ya Kitaifa nchini Kenya”. Deiksisi “mimi” ilidhihirisha mamlaka ya binafsi katika (31a) na (b), ikiwatoa Marais Kikwete na Samia kutoka katika hali ya sasa na kuwawakilisha katika njia iliyo rasmi zaidi. Aidha, uwepo wao katika nchi ya Kenya katika vipindi tofauti vya uongozi wao. Pia, walijitenga na wengine ili kuwajibikia wajibu wao katika kuimarisha uhusiano kati ya Kenya na Tanzania. Vilevile, kuendeleza sifa zao chanya kama muundomakro uliohalalisha matendo yao mtawalia. Mamlaka haya yalihalalisha na kujenga sifa chanya za wahutubu, pamoja na kibali cha kuzungumza, kuwa na hulka fulani, na kufanya maamuzi fulani.

Ujuzi wa Kitaaluma

Uhalalishaji huu hutokana na mtazamo au kurejelewa kwa kundi au taasisi ya taaluma bali si hadhi ya mtu binafsi katika jamii (van Leeuwen, 2008). Tazama madondoo ya (32a) na (b) hapa chini yanadhihirisha uhalalishaji kupitia mamlaka ya kitaaluma katika hotuba teule:

(32a) Vyombo vya ulinzi na usalama (Intelligence Services and Police Force) vya nchi zetu mbili vina ushirikiano wa karibu (ukurasa wa 7).

(b) Kwa hivyo, kupitia Kamati ya Wataalamu niliyoiunda, tumeanza mchakato wa kutafakari mbinu zaidi za kukabiliana na janga hili. (Heko) Tunapoendelea kusubiri mapendekezo ya wataalamu na hatua za kuchukua tahadhari zote, ikiwemo kusitisha baadhi ya safari kwenye maeneo ya mikurupuko zinachukuliwa (ukurasa wa 10).

Uhalalishaji kupitia mamlaka ya kitaaluma katika dondoo la (32a) ulifanikishwa kupitia kifungu, “vyombo vya ulinzi na usalama”. Kwa mujibu wa Wang (2022) katika diskosi za kisiasa taaluma huainishwa moja kwa moja. Mfano, kutaja kitambulisho cha wanasiasa cha ujuzi wa kitaaluma, hasa pale taaluma hiyo ilipofahamika kwa hadhira. Vyombo vya ulinzi na usalama hutafuta wahalifu na kuwakamata na vilipewa msisitizo zaidi kupitia kifungu “Intelligence Services and Police Force” (Ujasusi na Jeshi la Polisi). Kwa mujibu wa Reyes (2011) uhalalishaji hujumuisha mfumo ambao mzungumzaji hutoa kibali cha hulka fulani ya kijamii. Urejeleaji wa sekta ya ujasusi na jeshi la

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3591

polisi ulihalalisha ushirikiano wa kiusalama kati ya mataifa ya Kenya na Tanzania ili kukabili matukio ya ugaidi.

Kwa mujibu wa Said (2017) uhalalishaji hupatikana mhutubu anapotoa hoja fulani kufafanua maamuzi, maoni au tabia ambayo hadhira huenda isikubaliane nayo au isiiunge mkono. Ufafanuzi huu huunga mkono matendo, tabia au maamuzi ili kupata ukubalifu na hadhira. Yalikuwa mazoea ya kijamii kuwa matukio ya kigaidi yamewahi kutokea katika mataifa ya Kenya na Tanzania. Mojawapo wa matukio haya ni shambulizi dhidi ya Balozi za Marekani nchini Kenya na Tanzania mwaka 1998 na wanamgambo wa Al-Qaida. Kulikuwa na haja ya vyombo vya ulinzi na usalama kushirikiana ili kuepusha matukio kama haya kutokea tena. Hadhira ilipaswa kuunga mkono ushirikiano huu kwa sababu ulifanya na wataalamu ambao walishughulikia masuala ya usalama na ulinzi.

Fairclough (2011) anafafanua namna hejemonia husheheni michakato ya mazoea ya kijamii ambayo ni sehemu ya mchakato mpana wa kijamii na kitamaduni husaidia katika kuendeleza na kuzalisha hali za kijamii kitabaka. Hadhi ya Bwana Kikwete ya kuwa Rais ilimpa mamlaka ya kihejemonia. Kwa kurejelea vyombo vya usalama na ulinzi katika kuzuia uhalifu wa mipakani na ugaidi alihalalisha juhudi za kuzuia uovu huu. Juhudi hizi ziliendeshwa na wataalamu wa masuala ya ulinzi. Kwa mujibu wa nadharia ya uchanganuzi makinifu wa diskosi uhalalishaji hujumuisha michakato ya mazoea ya kijamii ya kuunda ukubalifu katika diskosi au mpangilio wa diskosi (Olga, 2013). Tishio la ugaidi na uhalifu wa mipakani kati ya mataifa ya Kenya na Tanzania lilisawiriwa na Rais Kikwete kama matukio ya mazoea ya kijamii. Ilikuwa bora likabiliwe na wataalamu katika vyombo vya ulinzi na usalama. Ili kuhalalisha ujitoleaji wa mataifa ya Kenya na Tanzania katika kupambana na wahalifu na magaidi wa kimataifa.

Aidha, Rais Samia alitumia mkakati wa uhalalishaji wa kupitia mamlaka ya ujuzi wa kitaaluma. Istilahi, "wataalamu" katika dondoo la (32b) ndio linalokuza uhalalishaji huu. Wataalamu walikuwa katika kundi lililobuniwa kushauri Taifa la Tanzania kuhusu namna ya kukabiliana na Korona-19. Walikuwa utaalamu wa kiafya na mapendekezo yao yangetumika kukabiliana na ugonjwa huu. Kwa mujibu wa van Leeuwen (2008) uhalalishaji huhusiana na mamlaka, hasa katika kuthibitisha mchakato ambao huchukuliwa ili kulinda uhalali wa matendo ya taasisi. Hivyo uhalalishaji huu ni uthibitishaji wa michakato ya taasisi. Wataalamu walitajwa ili kuwekea uzito juhudi zilizokuwa zikifanywa na Rais Samia katika kukabiliana na ugonjwa huu. Matendo ya wataalamu huhalalisha mchakato wa kijamii (Reyes, 2011), na katika muktadha huu yangehalalisha hatua za kupambana na Korona-19.

Kwa mujibu wa Shelby (2003) itikadi ni imani ambazo zinaweza kufanya mawazo potofu yawe ukweli. Dondoo la (32b) lilifafanuliwa kwa msingi kuwa May 2020 Hayati Rais Magufuli alitangaza kuwa Tanzania haikuwa na ugonjwa wa Korona-19. Shule zilifunguliwa na maisha yakaendelea kama kawaida, huku akipendekeza kuwa sala na miti shamba ni suluhu la ugonjwa huu. Baada ya kifo cha Hayati Rais Magufuli mwaka 2021 mageuzi kadhaa yalifanywa. Hata hivyo, kushawishi umma haikuwa rahisi kwa sababu ya kuambiwa na Hayati Magufuli kuwa ugonjwa wa Korona-19 haukuwepo nchini Tanzania (Selenya, 2024). Uhalalishaji huu ulidhihirisha kuwa Rais Samia alikuwa na mtazamo tofauti wa kiitikadi na ule wa Hayati Magufuli.

Kwa mujibu wa van Dijk (2006) uhalalishaji hutokea katika mazingira maalumu ambayo huchangiwa na muktadha na ung'amuzi wa vipengele vya kijamii. Mhutubu awe katika nafsi ya mamlaka na shughuli ya mawasiliano inaweza kupelekea kuwepo kwa hali ya ukosefu wa usawa wa kijamii ikiwa ni kwa maslahi ya mhutubu. Ingawa dondoo la (32b) lilionyesha kukiri kuwepo kwa ugonjwa nchini Tanzania, Rais Samia alikuwa Makamu wa Hayati Rais Pombe Magufuli ambaye alipinga uwepo wa Korona nchini humo. Hivyo,

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3591

uhalalishaji ni dhana ya uchanganuzi makinifu wa diskosi ambayo hurejelea namna usemi na diskosi huundwa na kuthibitisha michakato ya kijamii (van Dijk, 2006).

Ugonjwa wa Korona-19 ulikuwa tukio la kisiasa, Al-mwzaiji (2021) anaonya dhidi ya kuondoa Korona-19 kutoka kwa siasa kwa sababu juhudi za kukabiliana na ugonjwa huu zilikuwa za kisiasa. Hivyo, ugonjwa huu na juhudi za kuukabili lilikuwa suala la kisiasa. Hatua za serikali za kukabili msambao wake zilitegemea mwelekeo wa wataalamu wa afya bali si mtu binafsi au serikali bila kuzingatia maoni ya wataalamu. Rais Samia kwa kubuni kamati hii ilikuwa hatua ya kushirikiana na wataalamu katika taaluma yao. Hali hii iliipa taarifa yake ukubalifu kwa sababu ilionyesha kuwa angefanya maamuzi kutokana na nafasi ya kuwa na maarifa. Hatua ambazo zingefuata zingefaulu kwa sababu ziliidhinishwa na watu wenye utaalamu wa kiafya.

Ukaguzi wa madondoo ya (32a) na (b) ulibainisha kuwa yalihalalisha masuala ambayo hadhira huenda walikuwa na maarifa ya awali kuwa wahutubu hawakuwa na ufahamu nao na walihitaji kuwarejelea wataalamu. Aidha, wataalamu walitajwa ili kuhalalisha kitendo cha kushirikisha wanasiasa. Kushirikishwa kwa wanasiasa kulirejelewa ili kuhalalisha mchakato wa kijamii (Reyes, 2011). Urejeleaji huu uliashiria kuwa uamuzi ulifikiriwa na kutekelezwa kimakusudi na haukupaswa kupuuzwa. Mkakati wa uhalalishaji wa kutumia mamlaka ya ujuzi wa kitaaluma ulihalalisha masuala muhimu ya hotuba teule katika madondoo ya (32a) na (b) mtawalia. Marais Kikwete na Samia walirejelea taasisi au kamati ya ujuzi wa kitaaluma mtawalia ili kuhalalisha maamuzi yao bali si mtu aliyesimamia wajibu fulani. Zilirejelewa kwa sababu ya urasmi wake na uhalali wake kisheria, au zilichukuliwa kuwa na maarifa kuhusu suala fulani.

Mfano wa Kuigwa

Mtu ambaye ni mfano wa kuigwa anaweza kuwa mwanakundi wa kundi la “sisi” au watu mashuhuri ambao hulka zao au imani zao hufuatwa. Tazama hapa chini madondoo ya hotuba teule (33a) na (b) yanadhihirisha uhalalishaji wa mamlaka ya mfano wa kuigwa:

(33a) Nilipofika, Rais Kibaki akaniambia mambo mawili; kwanza, nimwambie Kofi Annan asiondoke kwani wakati huo walikuwa wameshavunja mazungumzo (ukurasa wa 6).

(b) Kama alivyowahi kusema Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alisema na ninanukuu: “Tukipoteza muda mwingi kugawana kibaba - kibaba ni kipimo cha kupimia kama mchele, ngano, sembe.” Anasema tukipoteza muda mwingi kugawana hicho tutapoteza muda mzuri sana wa kuvuna kipimo kikubwa zaidi (ukurasa wa 8).

Kwa mujibu wa Brunkert na Soest (2023) uhalalishaji kupitia mamlaka ya mfano wa kuigwa ni njia ya kuthibitisha kitendo, sera au awamu ya uongozi kwa kurejelea mamlaka ya uongozi, watu mashuhuri, mzazi au mwalimu. Kofi Annan alihalalisha kuja kwa Rais Kikwete nchini Kenya. Koffi Annan alipata umaarufu nchini Kenya kutokana na kuongoza ujumbe wa wapatanishi wa pande pinzani kuhusu uchaguzi wa urais baada ya Uchaguzi wa mwaka 2007. Mkakati wa uhalalishaji ulithibitisha msimamo wa Kikwete kuomba kuja baada ya pande hizi kukosa kuridhiana.

Kwa mujibu wa van Dijk (2006) urejeleaji wa mtu mashuhuri una changamoto kwa sababu inaweza kuifanya hadhira kughilibiwa kwa urahisi. Watu wanapohimiza nafasi, nguvu, mamlaka au ubora wao wa kimaadili hufanya hadhira kuamini, hata kama hawatoi ushahidi (Hansson & Page, 2022). Uhalalishaji huu ni udanganyifu ikiwa ungetumika kukwepa mjadala usio na mitazamo ya kibinafsi. Hauangazii ubora wa madai ya mhutubu bali huathiri hisia na mielekeo ya kijamii ya hadhira.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3591

Rais Kikwete hakueleza kwa nini yeye pekee ndiye angetumwa na Rais Kibaki. Kutowepo kwake kungemaanisha kuwa Kofi Annan angeondoka na amani haingepatikana na nchini Kenya. Rais Kikwete alihalalisha kutumwa kwake na Rais Kibaki kumwambia mkuu wa jopo la upatanishi Kofi Annan asiondoke.

Uchanganuzi makinifu wa diskosi ni mtazamo wa wingi-taaluma ambao hujikita kwenye uhusiano kati ya lugha, diskosi na mamlaka. Mtazamo huu huichukulia lugha kama mojawapo wa mchakato wa jamii (Fairclough, 2006). Muktadha wa kijamii hubainisha kinachosemwa na nani na wapi (Wodak, 2001). Dondoo hili lilidhihirisha mahusiano ya uwezo kati ya Marais Kikwete na Kibaki wakati huo. Rais Kikwete alitumwa kwa sababu alikuwa mwenza wa Rais Kibaki. Kwa maneno mengine ingawa kura za urais zilikuwa na utata, yeye alikuwa Rais. Kwa mujibu wa Fairclough na Fairclough (2012) uhalalishaji ni itikadi katika ukawaida wake. Huhusisha mifumo ambayo mipaka ya kiitikadi huunganishwa na taasisi hutekeleza majukumu yake kwa kupata uungwaji mkono wa kijamii. Rais Kikwete alikuja nchini Kenya kutokana na ujirani mwema kati ya mataifa haya na alipofika akatwikwa jukumu la kuchangia katika upatanishi.

Uhalalishaji huhusiana na mamlaka, hasa katika kuthibitisha mchakato ambao huchukuliwa ili kulinda uhalalishaji wa matendo ya taasisi (van Leeuwen, 2007). Hivyo, uhalalishaji ni kuthibitisha michakato ya taasisi. Dondoo la (33b) lilidhihirisha matumizi ya uhalalishaji wa mamlaka ya mfano wa kuigwa kupitia kifungu, “Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere” katika hotuba teule ya Rais Samia. Sauti ya mrejelewa iliwasilishwa kupitia usemi halisi ili kuhalalisha pendekezo lake la kuwa na soko la pamoja kwa watalii kati ya Kenya na Tanzania. Kwa mujibu wa Ivan (2009) umaarufu na ukubalifu wa msimamo fulani hutokana na kuungwa mkono na watu mashuhuri katika mawanda ya kijamii. Urejeleaji wa watu katika sekta fulani hufuatiwa na vitambulisho vya majina ya heshima. Tadmini ya onomastiki, “Baba wa Taifa” na “Mwalimu” ilifafanua kuwa istilahi hizi ilirejelea Rais mwanzilishi wa Taifa la Tanzania.

Kwa mujibu wa Kostova (2020) ni muhimu kwa mhutubu wa kisiasa kurejelea mtu mashuhuri kutoka kwa chama chake cha kisiasa ili kudhihirisha kuwa uliendana na uliungwa mkono na mamlaka makubwa ya kisiasa. Huenda Rais Samia alimnukuu Mwalimu Nyerere kuonyesha muwala wa kiitikadi wa CCM na sera za ujamaa za kuweka juhudi za kila mwanajamii pamoja ili kupata mafanikio ya kila mwanajamii. Hii ni kwa sababu uhalalishaji ni mchakato ambao kupitia kwake washiriki katika diskosi huunga mkono tukio au hulka kwa hadhira lengwa (Wang, 2022).

Kwa mujibu wa Shakoury (2018) jazanda ni kulinganisha vitu viwili visivyohusiana moja kwa moja au matukio ili kufafanua sifa za vingine. Neno “kibaba” lilitumiwa kijazanda kumaanisha kipimo kidogo cha watalii, yaani watalii wachache waliotembelea mataifa ya Kenya na Tanzania. Yalipaswa kuja pamoja ili kuwa soko moja la utalii ili kuvuna kipimo kikubwa zaidi. Kuunganishwa kwa masoko haya kungekuwa na faida kuliko kila taifa kuwa na soko lake la watalii. Jazanda hii ilimsawiri Rais Samia kama mtetezi wa kuwepo kwa soko la pamoja ili kupunguza hasara ya kutokuwepo kwa soko hilo. Aidha, alipinga mfumo wa kujisimamia ulioendelezwa na serikali hizi. Pia, alionekana kama kiongozi aliyeweka kipaumbele uwepo wa soko la pamoja la watalii.

Kwa mujibu wa Zheng (2000) mkakati wa kujumuisha hutokana na wanasiasa kujaribu kushawishi hadhira kuwa wao na hoja zao, “zilishughulikia maslahi ya watu.” Lengo lake huwa ni kumweka mhutubu katika kundi au vikundi, na kupata uungwaji mkono na kundi husika. Uhalalishaji huu ulileta hadhira kwa pamoja chini ya maoni ya “...Baba na Mwalimu...” wa nchi ya Tanzania. Ni mazoea ya kijamii kuwa “baba” na “mwalimu” kuheshimiwa katika jamii. Kwa mujibu

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3591

wa van Dijk (2003) uchanganuzi makinifu wa diskosi huchunguza mazoea ya kijamii ya kutokuwa na usawa, ukosefu wa haki, matumizi mabaya ya mamlaka na nguvu ambayo hutokana na diskosi yenyewe. Maoni ya Mwalimu Nyerere yalipaswa kutiliwa maanani kwa sababu uhalalishaji huunda imani na maadili mema ya pamoja ambayo hupendekeza, mkondo wa kutekeleza shughuli ili iwe halali (Fairclough na Fairclough, 2012).

Kwa mujibu wa van Leeuwen (2007) aina yote ya mamlaka hukuza imani katika mikakati ya uhalalishaji na uteuzi wa lugha huwa jukumu muhimu la lugha katika mchakato wa uhalalishaji. Istilahi zilizodhihirisha urejeleaji watu mashuhuri katika kauli za madondoo ya (33a) na (b) zilitekeleza majukumu ya kurejelea watu mashuhuri kutokana na maarifa ya awali kuhusu mtu maarufu aliyetajwa. Umaarufu wake ulikuwa bado katika kumbukumbu za hadhira. Aidha, waliorejelewa kama watu maarufu katika kuhalalisha tukio fulani waliangaziwa kwa njia chanya ambazo zilimpa uanachama wa kundi teule la mhutubu wa hadhira. Pia, uhalalishaji huu ulimwondolea aibu mhutubu kwa sababu ya vitendo vya awali ambavyo havikutolewa maelezo zaidi kwa hadhira. Hivyo, kuwepo kwa uwakilishinafsi chanya wa mhutubu.

Yasiyo ya Binafsi

Kwa mujibu wa van Leeuwen (2007) sheria, kanuni, amri, sera na taratibu au taasisi ni mkakati wa uhalalishaji wa mamlaka yasobinafsi. Uhalalishaji huu hutegemea dhana kuwa mamlaka yasobinafsi ni taasisi zinazojitegemea na hazihitaji kushikilia mpangilio fulani mkuu wa kimaadili (van Leeuwen na Wodak, 1999). Aidha, aina hii ya uhalalishaji hujibu swali, “kwa nini?” Data ya utafiti huu ilisheheni matumizi ya uhalalishaji kupitia mamlaka yasobinafsi katika hotuba teule tazama hapa chini:

(34a) Nakushuru zaidi kwa kunipa nafasi hii wakati ambapo nimebakisha siku chache kumaliza kipindi changu cha uongozi wa nchi yangu, kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu (ukurasa wa 6).

(b) kwa upande wetu tuko mbioni kukamilisha ujenzi wa kipande cha Pangani-Bagamoyo na barabara za lami zenye urefu wa kilomita 124.5. Tayari tumekwisha pata fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika. Jana nilikuwa na mazungumzo na kaka yangu Uhuru naye anamalizia mazungumzo ya kupata fedha ili kazi hii ianze kwa upande wa Kenya na tukutane pale kwenye mpaka (ukurasa wa 8).

Istilahi “katiba” katika dondoo la (34a) iliendeleza uhalalishaji kupitia mamlaka yasiyo ya binafsi katika hotuba teule ya Rais Kikwete. Kwa mujibu wa Foucault (1976) katiba huwasilisha, huendeleza na husimba turathi na itikadi za jamii. Katiba ni mhimili mkuu wa nguvu na hutawala diskosi za kisiasa. Kustaafu kwa Rais Kikwete kutoka mamlakani kulieleweka kwa msingi kuwa Rais Kikwete alikuwa katika sehemu ya mwisho wa muhula wa pili wa uongozi wake. Aidha, kifungu, “katiba ya nchi yetu”, kiliashiria kuwa ni kwa mujibu wa nchi ya Tanzania ambayo alikuwa akiiongoza. Pia, maana ya kifungu hiki ni nchi ya Tanzania ni taifa huru linaloongozwa na Katiba. Liliendesha shughuli zake za kiutawala bila shinikizo za kimataifa.

Uhalalishaji hujengwa kwa msingi wa kutii sheria na ni sababu ya kuthibitishwa hadharani na hutoa fursa kwa makubaliano ya jamii (Fairclough na Fairclough, 2012). Rais Kikwete alitii Katiba ya nchi ya Tanzania iliyompa uhalali wa kisheria kuongoza na kuwepo kwake mamlakani. Kwa mujibu wa Reyes (2011) kila kitendo cha kuhalalisha hupendekeza juhudi za kulipa kibali “tendo” au kutokuwepo kwa “tendo” au msimamo wa kiitikadi. Dondoo la (34a) lilidhihirisha itikadi ya Rais Kikwete kuhusu turathi za kidemokrasia kwa kutokatalia mamlakani. Kulingana na Shelby (2003) itikadi ni imani na sheria zinazotumiwa kughilibu na kushawishi watu kwa maslahi ya kundi tawala katika jamii. Rais Kikwete alikuwa mzalendo na aliheshimu sheria za nchi ya Tanzania.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3591

Kwa mujibu wa Olga (2013) uchanganuzi makinifu wa diskosi hujikita katika mikakati ya mazoea ya kijamii inayotumiwa na watu wenye mamlaka kushinikiza na kushawishi wengine kwa kusaidiwa na vipengele fulani vya kiisimu. Hadhira ya hotuba teule haikuishi katika ombwe. Huenda walikuwa na ufahamu wa Marais wanaosalia mamlakani kwa nguvu au kubadili katiba ili kujiongezea vipindi vya kuhudumu. Chilton (2004) anadokeza kuwa mawasiliano ya kisiasa husheheni malengo fiche ya utamaduni wa taifa. Uangaziaji wa malengo ya kijamii ni muhimu katika mfumo wa kuhalalisha, iliyo sehemu ya mawasiliano ya kisiasa. Uhalalishaji hushirikisha uwakilishinafsi chanya. Rais Kikwete alihalalisha kustaafu kwake kupitia kujitambulisha na kundi lililoenzi demokrasia.

Urejeleaji wa Benki ya Maendeleo ya Afrika ndio uliokuza uhalalishaji wa mamlaka yasiyobinafsi, yaani ni taasisi ya kifedha katika dondoo la (34b) kutoka kwa hotuba teule ya Rais Samia. Mkopo kutoka Benki hii ulihalalisha ujenzi wa barabara ya Lamu-Mombasa na Tanga-Bagamoyo hadi Dar-es-Salaam kupitia mkopo. Madu na wengine (2015) wanasisitiza kuwa lengo kuu la kupata mkopo kutoka kwa mashirika au mataifa ya kigeni ni kuboresha maisha raia, ujenzi wa miundombinu na kukuza uchumi. Madeni ya nje sio hasi kwa ujumla, ingawa kuna matumizi mabaya ya mikopo hii. Barabara hii ilikusudiwa kunufaisha mtagusano wa wananchi na usafirishaji wa bidhaa kati ya mataifa ya Kenya na Tanzania.

Kwa mujibu wa Reyes (2011) uhalalishaji katika hotuba za kisiasa unahitaji kupewa makini maalumu kwa sababu ni kutokana na hotuba hizi viongozi hutoa kibali kwa ajenda zao za kisiasa ili kuendeleza au kubadili mkondo wa taifa nzima. Dondoo la (34b) halikubainisha ikiwa pesa hizi zilikuwa za mkopo au la. Lilisisitiza kazi ambayo fedha zingefanya bila kutaja masharti ya kulipa mkopo huu. Huenda hadhira ilikosa maarifa yaliyohitajika au haikuweza au haikutaka kupinga au kuuliza ufafanuzi zaidi kuhusu mkopo huu. Huenda ni kutokana na kaida za bunge, makubaliano au malengo yaliyokubaliwa na raia wengine wa mataifa haya (Rojo na van Dijk, 1997). Kwa mujibu wa Awoyinfa na Taiwo (2010) baada ya kukamilika kwa ukoloni mkongwe Barani Afrika, mikopo inayotoka kwa mataifa ya dunia ya kwanza ni ukoloni mamboleo. Dondoo hili lilieleweka kwa msingi kuwa madeni ya kigeni yamepoteza umaarufu miongoni mwa mataifa ya nchi zinazoendelea.

Licha ya kuwa katika mfumo wa moja kwa moja, mamlaka hueleweka katika mfumo wa kushawishi, yaani matendo ya mtu huathiriwa kwa njia isiyo ya moja kwa moja kwa kushinikizwa kiakili kama vile imani, mielekeo na maarifa (van Dijk, 2015). Rais Samia katika dondoo la (34b) alijaribu kudhibiti akili za hadhira kwa kusisitiza masuala chanya kuhusu ujenzi wa barabara ili kupata uungwaji mkono na uhalalishaji wa kuchukua mkopo. Kundi lenye nguvu lina uwezo wa kupata habari katika jamii kuliko lisilokuwa nayo na huwa na uwezo wa kubainisha ni mada ipi na masuala yapi yangetolewa kwa umma (van Dijk, 2015).

Kwa mujibu wa van Rogers (2004) nadharia ya uchanganuzi makinifu wa diskosi haifafanui na kufasiri diskosi katika muktadha wa kijamii lakini hueleza kwa nini na namna diskosi hufanya kazi. Mkakati wa takwimu hutumiwa kushawishi na kusisitiza madai kwa kutumia nambari na takwimu (van Dijk, 1998). Takwimu za ujenzi wa barabara ya Pangani-Bagamoyo ya kilomita 124.5 haikupuuzwa kwa sababu ni ukweli usiopingika (Kostova, 2020). Benki hii ilileta dhana ya uhalalishaji wa mamlaka yasiyo binafsi.

Nadharia ya uchanganuzi makinifu wa diskosi huweka vipengele vya mazoea ya kijamii vinavyohusiana na tofauti na ukosefu wa usawa kati ya wanajamii (Meyer, 2001). Katiba na Benki ya Maendeleo ya Afrika zilihalalisha matukio ya kustaafu kwa Rais Kikwete na kukopa wa kujenga njia katika hotuba teule. Uhalalishaji huu ulihalalisha masuala yaliyokwisha kuamuliwa. Hadhira haikuwa na budi ila kuunga mkono

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3591

maamuzi yaliyochukuliwa. Katiba na Benki ya Maendeleo ya Afrika ilikuwa na mamlaka kuliko Marais. Ilihalisha hatua mahususi. Ilikuwa na mamlaka yasiyobinafsi.

Upatanifu

Mamlaka haya hutokana na , "kila mtu anafanya, na hivyo ndivyo nitafanya mimi". Ikiwa kila mmoja anafanya kitu fulani basi hakiwezi kuwa kibaya bali kinapaswa kuhalalishwa (van Leeuwen, 2007). Madondoo ya (35a) na (b) katika hotuba teule yanadhihirisha mamlaka upatanifu, tazama hapa chini:

(35a) Tunashirikiana kwa pamoja. Tunashirikiana kwa pamoja kama vile majambazi wakiiba kule wakikimbilia huku na wakiiba huku wakikimbilia kwetu. Sisemi ni tatizo la pamoja. Tatizo sasa limekuwa dunia nzima (ukurasa wa 7).

(b) Tunatambua kwamba kila nchi - ikiwemo Tanzania - imejiwekea utaratibu wa kupambana na janga hili kulingana na mazingira yake mahsusi na hali ya kusambaa kwa ugonjwa huo katika nchi hizo. Niliwaeleza Watanzania katika Hotuba yangu katika Bunge la Nchi yetu - na ninapenda kurejelea hapa– kwamba, sisi Tanzania sio kisiwa (ukurasa wa 10).

Rais Kikwete katika dondoo la (35a) alihalalisha matukio ya majambazi wa mipakani wanaoiba Kenya na kutorokea nchini Tanzania au kuiba Tanzania na kutorokea nchini Kenya katika hotuba teule ya Rais Kikwete. Kifungu ".Tatizo sasa limekuwa dunia nzima." kilitumika kuhalalisha hali hii kwa sababu hili sio tatizo kwa Kenya na Tanzania pekee. Ulimwenguni mataifa yanayopakana mara nyingi hushuhudia hali ya majambazi kuiba katika nchi moja na kutorokea nchi jirani. Mkakati wa mamlaka upatanifu ulimfaa Rais Kikwete kukwepa uwajibikiaji wa vyombo vya ulinzi kwa kukosa kuwanasa majambazi. Ikizingatiwa kuwa alikuwa akizungumza kama Amiri Mkuu wa vyombo vya ulinzi katika nchi yake. Hangevilaumu kwa sababu angekuwa akijitambulisha katika njia hasi. Kwa mujibu wa van Dijk (2006) uteuzi wa istilahi katika diskosi hushirikisha uteuzi wa maneno chanya kurejelea "sisi" na maneno hasi kwa "wao". Istilahi, "majambazi" ilidokeza maovu ya waliofanya vitendo vya kiuhalifu.

Katika mikakati ya mtagusano huwa kuna uwakilishinafsi chanya wa *sisi* na wa wengine hasi (van Dijk, 2006). Mkakati wa mazoea ya kijamii wa uhalalishajinafsi katika kauli ya dondoo la (35a) ulisisitiza ujihalalishaji wenyewe. Mazoea ya kijamii ya udhibiti wa mamlaka yalitumika katika uhalalishaji huu na kutofautisha nguvu na mamlaka kati ya mhutubu na hadhira. Hali hii hutokana na uwakilishinafsi wa mhutubu uliombadili na kumhalalisha. Mamlaka ya upatanifu yalihalalisha hali ya Rais Kikwete na Rais Uhuru kukosa kukomesha ujambazi wa mipakani kwa sababu hulka hii ilipatikana katika mataifa mengine ambayo si Kenya na Tanzania tu. Ni njia moja ya Rais Kikwete kukiri kuwa huenda alikosa namna ya kumaliza uhalifu huu licha ya juhudi kuwekwa. Dondoo hili liliendeleza hadhi ya kijamii ya kundi la majambazi. Juhudi za kuyakabili zilitaka ushirikiano wa kimataifa kati ya mataifa mbalimbali bali si taifa moja.

Uchanganuzi makinifu wa diskosi huchunguza ukosefu wa usawa katika usemi. Diskosi huakisi kwa namna miundochangamani huhalalisha na kuzalisha upya mahusiano ya uwezo na utawala (van Dijk, 2008). Istilahi, "jambazi" iliwaweka wahalifu katika kundi la "wao" kutokana na mahusiano na iliharamisha vitendo vyao vya kiuhalifu. "sisi" walikuwa waathiriwa wa matendo ya majambazi. Mkakati wa kutowataja waliorejelewa kwa majina ulithibitisha kuwa uhalifu wa mipakani ulikumba mataifa yote, jambo lililokuwa sehemu ya mamlaka ya upatanifu. Mfumo huu wa mazoea ya kijamii wa kuficha na kutenga ulipunguza mamlaka na kuharamisha "wao". Rais Kikwete alikuwa na ukiritimba wa maarifa kuhusu ukweli wa hali ya majambazi wa kimataifa ulimwenguni.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3591

Kifungu, “kila nchi - ikiwemo Tanzania.” katika dondoo la (35b) kilihalalisha kwa mamlaka ya upatanifu katika hotuba teule ya Rais Samia. Ilidhihirika kuwa sio nchi ya Tanzania tu ndio iliweka utaratibu wa kupambana na ugonjwa wa Korona-19. Utaratibu huu ulitegemea mazingira na hali ya msambao wa ugonjwa huu katika nchi hizo. Kulikuwepo na utaratibu wa kuzuia ugonjwa huu jinsi ilivyo katika mataifa mbalimbali katika ulimwengu mzima.

Kwa mujibu wa van Dijk (2015) wenye mamlaka wanaweza kukosa kuyatumia lakini yanaweza kudumishwa kupitia matendo ya kawaida ya kila siku. Dondoo la (35b) lilibainisha mabadiliko ya ghafla kwa uongozi wa Tanzania baada ya kifo cha Hayati Rais Magufuli. Kauli ya dondoo hili ilieleweka kuwa baada ya mkurupuko wa ugonjwa wa virusi vya Korona-19 mataifa mbalimbali yaliweka utaratibu za kuzua msambao wake. Hayati Magufuli alipuuza mikakati na taratibu zilizopendekezwa na Shirika la Afya Dunia (WHO) na kutangaza kuisha kwa Korona-19. Aidha, alipinga matumizi ya chanjo akidai kuwa ilikuwa sehemu ya ukoloni wa nchi za Kimagharibi kwa Afrika (Salenya, 2024). Dondoo la (35b) lilidhihirisha mtazamo mpya wa serikali ya Tanzania kuwa na utaratibu wa kuzuia maambukizi zaidi. Aidha, kwa njia isiyo ya moja kwa moja alikiri kuwepo kwa ugonjwa huu nchini Tanzania.

Uhalalishaji ni dhana ya uchanganuzi makinifu wa diskosi inayorejelea namna usemi na diskosi hujenga na kuthibitisha michakato ya kijamii (van Dijk, 2009). Dondoo la (35b) lilidhihirisha kuwa Rais Samia alikuwa mamlakani na hivyo katika mahusiano ya uwezo alikuwa na mamlaka kuliko Hayati Magufuli kwa sababu alibadili sera zake. Kwa mujibu wa Rojo na van Dijk (1997) mamlaka ya upatanifu hujumuisha uhalalishaji wa kimaadili na balagha ya kutokuwa na msimamo ya kibinafsi. Tofauti na mtu mwenye mtazamo tofauti asiyewakilisha uhalisia, uhalalishaji binafsi wa mhutubu hudai kuwa anayowasilisha si tafsiri ya kibinafsi bali ni uhalisia. Hali hii humsawiri mhutubu kuwa mwenye uhalali wa kimaadili wa kutegemewa na kuaminiwa. Uhalisia katika kipindi cha kutolewa kwa hotuba teule ni kuwa mataifa mengi yalikuwa na taratibu za kuzuia ugonjwa huu. Ilikuwa hatua ya kimaadili kwa taifa la Tanzania kuwa na utaratibu kama huu.

Madondoo ya (35a) na (b) yalibainika kuwa Marais Kikwete na Samia walitumia ujitoleaji binafsi na makubaliano ya pamoja katika kukuza dhana ya mamlaka upatanifu. Mkakati wa kujitolea ulihalalisha upatanifu katika kuendeleza ukubalifu na hivyo kuonyesha kuwa walikuwa wa kuaminika na wenye misimamo dhabiti. Ulidhihirisha ushiriki wao wa binafsi na uwajibikiaji wa kupambana na majambazi wa mipakani na ugonjwa wa virusi vya Korona-19 mtawalia. Pia, uundaji wa makubaliano na umoja, ambao ni mkakati wa uhalalishaji wa mamlaka upatanifu katika madondoo ya (35a) na (b), ulifikiwa kupitia dhana ya *sisi* na *wao* ya kiuhasama. *Sisi* ni waliokuwa wakipigana na uhalifu wa mipakani na walioweka taratibu za kuzuia msambao wa ugonjwa wa virusi vya Korona-19 mtawalia. “Wao” ni majambazi waliowafanya uhalifu wa mipakani na waliopuuza kuweka mikakati ya kuzuia maambukizi ya ugonjwa wa Korona-19.

Kimila

Istilahi kama vile “jadi”, “hulka” na “utamaduni” hushawishi hadhira kuhusu uhalali wa kitendo fulani. Ni machukulio ya kijamii kuwa “kwa sababu tumekuwa tukifanya hivi katika kipindi cha awali” hufanikisha kudai uhalali wa kitendo (van Leeuwen na Wodak, 1999). Hotuba teule zilidhihirisha matumizi ya uhalalishaji wa mamlaka ya kimila, kama inavyoonekana katika madondoo (36a) na (b) hapa chini:

(36a) Kila wakati kukitokea tukio la ugaidi watu wakiuawa na wengine wakiumia huwa nampigia Rais simu na kumpa (ukurasa wa 7).

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3591

(b) Busara inaelekeza kuwa ukiwa mpangaji mpya kwenye eneo lazima ujitambulishaji kwa majirani (ukurasa wa 5).

Kifungu, ".kila wakati." kilikuza uhalalishaji wa mamlaka ya kimila katika dondoo la (36a). Mofu {ni} katika kitenzi, "(ni)nampigia" ilimtambulisha Kikwete kuwa Rais wa Tanzania. Ujitambulishaji huu ulimweka katika kundi moja la waathiriwa wa vitendo vya kigaidi. Aidha, alikuwa mwakilishi wa kutuma pole kwa taifa la Kenya kupitia Rais Uhuru kwa sababu ya wao kuwa na hadhi sawa ya kijamii. Dondoo hili lilihalalisha mazoea ya Rais Kikwete kumpa Rais Uhuru pole kila tukio la kigaidi lilipotokea nchini Kenya.

Diskosi hutegemea muktadha wa kihistoria, semi hupata maana kutokana na muktadha mahususi wa kijamii, kitamaduni na kiitikadi pamoja na wakati na sehemu ya tukio (Wodak, 1996). Dondoo la (36b) lilieleweka kwa msingi kuwa kipindi cha miaka mitatu kufikia mwisho wa mwaka 2015, Kenya ilishuhudia mashambulizi hamsini yaliyotokana na wanamgambo wa Al-Shabaab kulingana na vyombo vya habari wakati huo. Shambulizi lenye maangamizi makubwa katika kipindi hiki lilitokea tarehe 2/4/2015 katika Chuo Kikuu cha Garissa, watu 148 waliuawa wakiwemo wanafunzi 142 (Eboi, 2015). Kisa hiki kiliangaziwa na vyombo vya habari nchini Kenya na Kimataifa. Rais Kikwete alikuwa na ufahamu wa shambulizi hili kwa sababu lilitokea muda mfupi kabla ya kutolewa kwa hotuba teule. Hali hii ilifafanua kwa nini Rais Kikwete alitumia kifungu cha maneno, "kila wakati" ili kurejelea utokeaji wa visa vya kigaidi chini ya uongozi wa Rais Uhuru.

Kwa mujibu wa Wodak (1996) kila mhutubu hutumia ujuzi wa mazoea ya kijamii ambayo hutimiza maslahi na malengo ya kipekee na husheheni utengaji na ujumuishaji. Uhalalishaji kupitia mamlaka ya kimila ulimpa Rais Kikwete fursa ya kujumuisha vitendo vya kigaidi vilivyotendeka nchini Kenya chini ya uongozi wa Rais Uhuru katika kundi moja bila kuvirejelea moja kwa moja. Aidha, ulitenga vitendo vingine vya kigaidi ambavyo viliwahi kutendeka nchini Kenya kabla ya uongozi wa Rais Uhuru, na hivyo kuhalalisha 'kupeana pole' kuhusu mashambulizi ya kigaidi chini ya uongozi wa Rais Uhuru.

Uchanganuzi makinifu wa diskosi huazimia kuchunguza miundo ya mahusiano ya uwezo, udhibiti na namna utawala, unavyoelezwa au kuhalalishwa katika diskosi (Weiss na Wodak, 2003). Rais Kikwete alionyesha huruma kupitia dondoo hili. Kwa mujibu Fairclough na Fairclough (2012) mamlaka hupeana idhini ya kutekeleza kitendo kwa sababu ya kutii mamlaka halali au kwa kukwepa au kutafuta matokeo fulani. Mkakati wa kuoneana huruma uliibua dhana kuwa Rais Kikwete alitarajiwa kupeana pole kila wakati kulikuwa na shambulizi la kigaidi nchini Kenya. Nchi za Kenya na Tanzania zilipakana na ukaribu huu ulimlazimu kukemea matukio ya kigaidi ili kudhihirisha ujirani mwema. Kwa mujibu wa van Dijk (1993) mamlaka yanaweza kudhihirishwa kupitia nguvu ili kudhibiti matendo au kupitia kushawishi au kughilibi. Uhalalishaji huu ulimtambulisha Rais Kikwete kama mmoja wa kundi la Wakenya waliokuwa waathiriwa wa mashambulizi ya kigaidi. Aidha, ulihalalisha nafasi yake kama kiongozi wa taifa jirani ambalo ni mshirika wa kimkakati.

Uwepo wa neno, "lazima" ulikuza dhana ya uhalalishaji kupitia mamlaka ya kimila katika dondoo la (36b) katika hotuba teule ya Rais Samia. Kwa mujibu wa Fairclough na Wodak (1997) uchanganuzi makinifu wa diskosi hufichua miundo ya mamlaka na michakato ya itikadi katika jamii kutoka kwa mtazamo wa kiisimu. Isitoshe, hutambulisha mikakati ya mazoea ya kijamii ambayo hutumiwa na washiriki wa kijamii katika diskosi kufikia malengo yao. Ni mazoea ya jamii kuwa mpangaji mpya kwenye eneo hujitambulisha kwa majirani ili kufahamiana na majirani yaani wenyeji.

Kulingana na Wodak (1996) nadharia ya uchanganuzi makinifu wa diskosi haifasiri tu

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3591

ujumbe bali hutoa maelezo. Istilahi 'mpangaji mpya' ilitumika kijazanda kurejelea Rais Samia, aliyetwaa uongozi kipindi kifupi kabla ya kutoa hotuba teule. Kwa mujibu wa Lakoff na Johnson (1980) kuwepo kwa jazanda ni kuelewa na kushuhudia aina moja ya kitu kwa niaba ya kitu kingine. Istilahi hii ililinganisha urais na upangaji wa nyumba. Kwa mujibu wa Kobia (2008) jazanda hukuza maoni, falsafa, matarajio, mielekeo, mitazamo, uelewaji na ufasiri wa masuala mbalimbali katika muktadha wa diskosi. Dhana hii ilieleweka kwa msingi kwamba mwenye nyumba humkodishia mpangaji kwa kipindi fulani cha wakati. Hivyo, katika dondoo hili wapangaji ni marais waliochaguliwa na wananchi kuongoza kwa kipindi mahususi. Dondoo la (36b) lilipata mantiki kuwa kutokana na utandawazi, dunia imekuwa kijiji na Rais Samia alijirejelea kama mpangaji kwa sababu ya taifa aliloongoza lilikuwa sehemu ya dunia, yaani kijiji.

Kwa mujibu wa van Leeuwen na Wodak (1999) kupitia diskosi washiriki wa kijamii husheheni maarifa, hali, majukumu ya kijamii. Vilevile, kuna ujitambulishaji na mahusiano ya kibinafsi kati ya makundi ya kijamii yanayoingiliana. Ujitambulishaji wa Rais Samia kama 'mpangaji mpya' na Rais Uhuru kama 'mpangaji mwenyeji' uliwaweka katika hadhi sawa ya mamlaka kwa sababu wote walikuwa wapangaji. Kuongoza taifa kulikuwa sawa na kukodi nyumba. Hata hivyo, ujitambulishaji huu ulieleweka kwa muktadha kuwa waliorejelewa kama “wenyeji” walikuwa na uzoefu wa namna ya kuendesha ushirikiano wa kikanda. Maarifa yao yalihitajika ili kubainisha njia mwafaka za kuimarisha ujirani. “Mpangaji mwenyeji” alikuwa na mamlaka zaidi kuliko “mpangaji mpya” kutokana na tajriba ya kuliongoza taifa kwa kipindi fulani. Ilimlazimu Rais Samia kumtembelea Rais Uhuru kwa sababu ni tendo la kimila la “mpangaji mpya” kumtembelea “mpangaji mwenyeji”.

Aidha, mifumo tofauti ya mamlaka aghalabu hutumia lugha kushawishi au kuhalalisha kwa nini walichukua au hawakuchukua hatua fulani (Alamri, 2017). Hatua ya Rais Samia kujirejelea kuwa “mpangaji” ilimtambulisha na hadhira ambayo baadhi yao huenda walikuwa wapangaji kindakindaki wala si wa kijazanda. Walifahamu uhusiano kati ya “mpaganji mpya” na “mpangaji mwenyeji”. Kuongoza taifa ilikuwa sawa na kukodi nyumba. Ikizingatiwa kuwa nchi za Kenya na Tanzania ni demokrasia. Wenye nyumba za kupanga walikuwa wananchi ambao walichagua serikali. Ni mazoea ya kijamii kuwa Marais katika nchi hizi huchaguliwa na wananchi na wao ndio huteua namna ya kutawala. Kwa mujibu wa Weiss na Wodak (2007) uchanganuzi makinifu wa diskosi huangazia namna itikadi huwekea mihimili mahusiano ya uwezo yasiyokuwa sawa. Kwa msingi huu umma ulipewa hadhi ya juu kuliko Marais kwa sababu wao ndio wenye uwezo wa kuamua ni nani angewaongoza kama mikakati ya kuighilibu.

Uhalalishaji wa mamlaka ya kimila katika kauli ya madondoo ya (36a) na (b) ulithibitisha kuwepo kwa hatua zenye sifa chanya. Kwa mujibu wa van Dijk (2001) diskosi za kisiasa hujukumika katika kukuza, kuzalisha upya na kuhalalisha mamlaka na utawala. Hadhi ya urais ya Rais Kikwete na Rais Samia iliwaunganisha na hadhira kama 'waathiriwa' na 'wapangaji' mtawalia. Hili lilifanyika ili kuhalalisha kwa mamlaka ya kimila ya kutoa pole na mpangaji mpya kumtembelea mpangaji mwenyeji katika jamii. Uhusiano huu ulihimizwa katika kiwango cha urais kama njia ya kuzingatia itifaki na kuonyesha heshima kwa uongozi uliokuwepo mamlakani.

HITIMISHO

Makala hii ilibainisha kuwa mkakati wa uhalalishaji wa mamlaka katika hotuba za Marais Kikwete na Samia ulifanyika kupitia kwa mamlaka ya kibinafsi, wataalamu, mfano wa kuigwa, yasiyo binafsi, upatanifu na kimila. Uhalalishaji huu ulibainisha kuwa maamuzi ya kisiasa ni halali tu iwapo yalifanywa kwa mfumo ambao ulikubalika na maadili ambayo yalithibitishwa na umma. Umahususi wa vitendo vya uhalalishaji ulitegemea hali mbalimbali za muktadha na ulihusiana na

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3591

michakato ya kuthibitisha ili kulinda uhalali wa matendo ya wahutubu au taasisi. Mkakati wa uhalalishaji wa mamlaka ulithibitisha michakato ya kitaasisi katika hotuba teule.

MAREJELEO

Alamri, E. H. (2017). Strategies of Legitimisation, The Case of Women Driving in Saudi Arabia (Unpublished PHD Thesis). Newcastle of University.

Al-Mwzaiji, K. N. A. (2021). The Political Spin of Conviction: A Critical Discourse Analysis of the Origin of COVID-19. *Journal of Language Studies*, *21*(1), 239–252. https://doi.org/10.17576/gema-2021-2101-14.

Awoyinfa, C. F., S. O., & Taiwo, A. A. (2010*). Foreign Debts in Africa and the Challenges of Democracy*. Enugu Publisher.

Bayley, P. (2004). *Cross-cultural Perspectives on Parliamentary Discourse*. John Benjamins Publishing Company.

Brunkert, L., & Soest, C. (2023). Praising the Leader: Personalist Legitimation Strategies and the Deterioration of Executive Constraints. Democratization, 30(3), 419–439. https://doi.org/10.1080/13510347.2022.2150760. Retrieved on 21/02/2025.

Bryman, A., (2016). *Social Research Methods 5th Edition*. Oxford University Press.

Cap, P., (2008). Towards the Proximization Model of the Analysis of Legitimization in Political Discourse. *Journal of Pragmatics*, 40(1), pp. 17-41.

Chilton, P. (2004). Analyzing Political Discourse: Theory and Practice, *Applied Linguistics Journal* 26(3), pp. 462-469.

Eboi, A. (2015). A Content and Critical Discourse Analysis of Nation Newspaper Coverage of the Garissa University College Terrorist Attact in Kenya. *Contemporary Social Science*. Vol. 24(3), pp. 137-165.

Fairclough, N. (1992). Discourse and text: Linguistic and intertextual analysis within discourse analysis. *Discourse & Society, 3*(2), 193– 217. https://doi.org/10.1177/0957926592003002004

Fairclough, N. (2006). *Language and Globalization*. Routledge.

Fairclough, N., Mulderrig, J. & Wodak, R. (2011). Critical Discourse Analysis. In T. A. van Dijk (ed), *Discourse Studies: A Multi-Disciplinary Approach* (pp. 357-378). London: Sage.

Fairclough, I., & Fairclough, N. (2012). *Political discourse analysis: A method for advanced students*. Routledge.

Fairclough, N., & Wodak, R. (1997). Critical Discourse Analysis. In: Ed. VanDjik, T. *Discourse Studies*: A *Multidisciplinary Introduction* (pp. 258-284). Sage Publications Ltd.

Foucault, M. (1976). *Histoire de la Sexualité: La Volonté du Savoir*. Paris: Gallimard.

Hansson, S., & Page, R. (2022). Corpus-Assisted Analysis of Legitimation Strategies in Government Social Media Communication. https://doi.org/10.1177/17504813221099202. Retrieved on 21/01/2025.

Huckin, T., Andrus, J., & Lemon, C. J. (2012). *Critical Discourse, Rhetoric and Composition*, National Council of Teacher of English, 64(1), pp. 107-129.

Jamil, N. (2014). Demonizing Demonstration: (De) Legitimation Strategies through Emotions in Speeches of Hosni Mubarak and Ben Ali, Middle East Journal of Scientific Research 20,

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3591

Language for Communication and Learning, pp. 1-10, ISSN1992-9222, IDOSI Publication.

Kobia, J. (2008). Metaphors on HIV/AIDS Discourse among Oluluhyia Speakers of Western Kenya, Critical Approaches to Discourse Analysis Across Discipline, http://cadaad.org/ejournal2(2): 48-66, ISSN: 1752-3079.

Kostova, B. (2020). Authority Legitimation in Campaign Discourse of American Presidential Candidates. *Studies in Linguistics, Culture, and FLT*, *8*(2), 52-84.

Madu, A.Y., wengine (2015). The Political Economy of External Debt Management in Nigeria: Strategies, Issues and Challenges. *Australia Journal of Basic and Applied Science*. Vol. 4(2), 46-64.

Mugenda, O. M., & Mugenda, G. A. (1999). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches*. Acts Press.

Olga, L. (2013). Discursive legitimation strategies in the media. Case study of the UK retail planning policy. [Unpublished Master dissertation]. Aalto University.

Reyes, A. (2011). Strategies of Legitimization in Political Disourse: from Words to Action, *Discourse & Society*. 22(6), pp. 781-807: Sage Publications Ltd.

Rogers, R. (2004). *An Introduction to Critical Discourse Analysis in Education*. New Jersey: Lawrence Erlbaum.

Rojo, L. M., & van Dijk, T. A. (1997). There was a Problem, and It was Solved!": Legitimating the Expulsion of 'Illegal' Migrants in Spanish Parliamentary Discourse. *Discourse & Society*, 8(4), 523–566.

Said, H. (2017). Legitimation Strategies in Egyptian Political Discourse: The Case of Presidential Speeches [Unpublished master's thesis]. The American University in Cairo.

Selenya, J.J. (2023). Strategies of (De)Legitimation of COVID-19 Vaccines in Tanzanian Political Speeches. Professional Discourse & Communication, 5(3), pp. 76– 92. https://doi.org/10.24833/2687-0126-2023-5-3-76-92.

Shakoury, K. (2018).Critical discourse analysis of Iranian Presidents' addresses to the United Nations General Assembly (2007-2016)(Doctoral dissertation). University of Saskatchewan.

Shelby, T. (2003). Ideology, Racism, and Critical Social Theory. *The Philosophical Forum*. Vol. (34), No.2, pp.153– 188. tommieshelby.com/uploads/4/5/1/0/45107805/ideology_and_racism.pdf. retrieved on 14 January, 2025.

van Dijk, T. (1991). *Racism and the Press: Critical Studies in Racism and Migration*. London: Routledge Publishing Company.

van Dijk, T.A., (1993). Discourse, Power and Access. In: C.R. Caldas (ed.). *Studies in Critical Discourse Analysis*. Routledge.

van Dijk, T. A., (1995). Aim of Critical Discourse Analysis, *Japanese Discourse Journal*, 1(1), pp. 17-28.

van Dijk, T. A., (1998). *Ideology: A Multidisciplinary Approach*. Sage Publications Ltd.

van Dijk, T. A., (2001). Critical Discourse Analysis, in: D. Schiffrin, D. Tannen and H.E. Hamilton (eds) *Handbook of Discourse Analysis*. Oxford Press.

van Dijk, T. A., (2002). Political Discourse and Political Cognition, in: P. Chilton & C. Schaffner (Eds), *Political as a Text and Talk: Analytic Approaches to Political Discourse*. John Benjamins Publishing Company.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3591

van Dijk, T. A. (2003). The Discourse-Knowledge Interface. In G. Weiss & R. Wodak (Eds.), *Critical Discourse Analysis: Theory and Interdiscipilinarity* (pp. 85–109). Palgrave Macmillan.

van Dijk, T.A. (2005). Politics, Ideology and Discourse: Elsevier Encyclopaedia of Language and Linguistics. In: R. Wodak (ed) *Volume on Politics and Language*. pp. 728-740.

van Dijk, T. A., (2006). *Principles of Critical Discourse Analysis*. Sage Publications Ltd.

van Dijk, T. A., (2008). *Discourse and Power*. Palgrave Macmillan

van Dijk, T.A., (2009). Critical Discourse Studies: A Sociocognitive Approach. In: R. Wodak, M. Meyer (eds). *Methods of Critical Discourse Analysis*. Sage Publications Ltd. pp. 62–86.

van Dijk, T. A. (2015). Critical Discourse Analysis. In D. Tannen, H. E. Hamilton, & D. Schiffrin (Eds.), *The Handbook of Discourse Analysis* (2nd ed., pp. 466–485). Wiley-Blackwell.

van Leeuwen, T. (2007). Legitimation in Discourse and Communication. *Discourse and Communication*. Vol. 1(1), pp. 91–112.

van Leeuwen, M. (2008). The Style of Political Speeches: Problems in Existing Method, retrieved from https://hdl.handle.net/1887/14678, retrieved on 8 June, 2024.

van Leeuwen, T., & Wodak, R. (1999). Legitimizing immigration control: A discourse-historical analysis. *Discourse Studies*, *1*(1), 83-118. https://doi.org/10.1177/1461445699001001005

Wang, Y. (2022). Legitimation Strategies in Political Rhetoric: Examples from Presidential Speeches on Covid-19. *Theory and Practice in Language Studies*. Vo. 12(5), pp. 894–903. https://doi.org/10.17507/tpls.1205.09.

Weiss, G., & Wodak, R. (Eds.). (2003). *Critical Discourse Analysis: Theory and Interdisciplinarity*. Palgrave Macmillan

Wodak, R. (2001). The Discourse-Historical Approach. In: R. Wodak & M. Meyer (eds), *Methods of Critical Discourse Analysis*, (pp. 63-94). Sage Publications Ltd.

Wodak, R. (1996). *Disorder of Discourse*. Longman.

Wodak, R., & Meyer, M. (Eds.). (2009). *Methods of critical discourse analysis* (2nd ed.). Sage.

Zheng, T. (2000). Characteristics of Australian political language rhetoric: Tactics of gaining public support and shirking responsibility. Journal of Intercultural Communication, 4. Retrieved December 21, 2024, from: www.immi.se/intercultural/nr4/zheng.htm.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.